JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAJI**

Simu: +255 (0) 26 2322602
Tovuti: www.maji.go.tz
Barua pepe: ps@maji.go.tz

Mji wa Serikali,
Mtaa wa Maji,
S. L. P. 456,
**DODOMA**.

Dodoma: Januari 30, 2026

**TAARIFA KWA UMMA**

Wizara ya Maji inawataarifu wadau wa sekta ya maji na umma kwa ujumla kuwa **Mkutano wa Mwaka wa Tisa (9) wa Bodi za Maji za Mabonde**, **Mkutano wa Saba (7) wa Jukwaa la Taifa la Wadau wa Sekta Mtambuka katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji**, pamoja na **Uzinduzi wa Bodi ya Tano (5) ya Taifa ya Maji**, umefanyika kwa mafanikio makubwa jijini Dodoma kuanzia tarehe **27 hadi 30 Januari, 2025**.

Mikutano hiyo ilifanyika chini ya kaulimbiu: **"Uhakika wa Maji kwa Maendeleo ya Taifa: Utekelezaji wa Dira 2050 katika Ustahimilivu, Usawa na Uendelevu."** Kaulimbiu hii ililenga kuhimiza na kuharakisha uwekezaji katika uhakika wa maji pamoja na kuimarisha utekelezaji wa usimamizi endelevu wa rasilimali za maji kwa kuzingatia mwelekeo wa **Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 (DIRA 2050).**

Mikutano hiyo iliwakutanisha **Bodi za Maji za Mabonde, Bodi ya Taifa ya Maji, Wizara ya Maji, Wizara na Taasisi zinazohusiana na maji, washirika wa maendeleo, taasisi za umma na binafsi, asasi za kiraia, vyuo na taasisi za utafiti, pamoja na wadau wengine wa sekta ya maji**, ambapo walijadili masuala ya kimkakati kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji, uwekezaji katika uhakika wa maji, na maendeleo endelevu ya taifa.

Katika Mkutano Mkuu wa Tisa wa Mwaka (AGM), washiriki walifanya **tathmini ya kina ya utendaji wa Bodi za Maji za Mabonde kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi 2025**, kubaini mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo, na kuweka **maazimio na mwelekeo wa kimkakati kwa kipindi kijacho**. Aidha, mkutano uliweka msisitizo katika kuimarisha usimamizi jumuishi wa rasilimali za maji (IWRMD), hususan katika kipindi hiki ambacho Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2026.

Vilevile, mikutano ilikubaliana juu ya umuhimu wa **kuoanisha mipango na utekelezaji wa sekta ya maji na mifumo mipya ya mipango ya maendeleo ya taifa**, ikiwemo **DIRA 2050, Mpango wa Mtazamo wa Muda Mrefu, pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2025/26–2029/30)**, ili kuhakikisha rasilimali za maji zinachangia kikamilifu ustahimilivu wa tabianchi, usalama wa chakula, nishati, viwanda, na uchumi wa kijani na buluu.

Mkutano huo pia ulishuhudia **hatua muhimu ya kitaasisi kupitia uzinduzi wa Bodi ya Taifa ya Maji ya Tano**, jambo linalodhihirisha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha misingi ya **utawala bora, uwazi, uwajibikaji na ufanisi** katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

Sambamba na hilo, **Mkutano wa Saba wa Jukwaa la Taifa la Wadau wa Sekta Mtambuka**

uliwezesha mjadala mpana kuhusu **mikakati ya kuimarisha uhakika wa maji nchini**, kwa kuzingatia mchango wa sekta mtambuka ikiwemo mazingira, afya, kilimo, nishati, mipango ya matumizi ya ardhi, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Washiriki walikubaliana juu ya umuhimu wa ushirikiano wa karibu kati ya sekta hizi ili kufanikisha uhakika wa maji wa muda mrefu pamoja na kuweka Mpango wa pamoja wa Uwekezaji katika Uhakika wa Maji.

Wizara ya Maji inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote, washirika wa maendeleo, na vyombo vya habari kwa ushiriki wao na mchango muhimu katika mikutano hii. **Maazimio na mapendekezo yaliyotolewa yatatumika kuongoza sera, mipango, na uwekezaji wa sekta ya maji**, kwa lengo la kuhakikisha uhakika wa maji na maendeleo endelevu ya taifa kwa kizazi cha sasa na kijacho.

**IMETOLEWA NA**;
KITENGO CHA HABARI

**30 JANUARI, 2025**